# SAUTI YA TSC

TOLEO NA. 32 JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC) OKTOBA 2023

# WAZIRI MCHENGERWA AWAONYA WATENDAJI WASIOWAJIBIKA, AAHIDI KUIREJESHA TAMISEMI KWA WANANCHI



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Mohamed Mchengerwa (Mb) akiongea na watumimishi wa Ofisi ya Rais TAMISEMI (hawapo pichani) mara baada ya kuwasili Ofisi za Wizara zilizopo Mji wa Kiserikali Mtumba jijini Dodoma tarehe 04 Septemba, 2023.*

**MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA**
**Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz**

Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania tumeyautumishiwawalimutanzania

# WATUMISHI TSC TUMUUNGE MKONO WAZIRI MCHENGERWA KWA KUONGEZA BIDII YA UTENDAJI KAZI

Tarehe 4 Septemba, 2023 Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Mohamed Mchengerwa alikaribishwa rasmi Ofisi ya Rais TAMISEMI baada kuteuliwa na kuapishwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kuongoza Wizara hiyo akitokea Wizara ya Maliasili na Utalii.

Katika hotuba yake wakati wa hafla ya ukaribisho, Waziri Mchengerwa aliwaonya watendaji wote wa Ofisi ya Rais TAMISEMI, Taasisi zinazosimamiwa na Ofisi hiyo, Tawala za Mikoa pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa ambao ni wabadhirifu, wala rushwa na wasiowajibika katika utendaji kazi wao kuwa hatawavumilia katika utendaji wake wa kazi.

Waziri huyo aliweka msisitizo kuwa anataka kuirejesha wizara hiyo kwa wananchi kwa kuhakikisha watendaji wote wanasikiliza na kutatua kero za wananchi kwa wakati.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ikiwa ni miongoni mwa Taasisi zinazosimamiwa na Ofisi ya Rais TAMISEMI inapaswa kuhakikisha inamuunga mkono Waziri Mchengerwa kwa kuongeza kasi na ubora katika kuwahudumia walimu.

Watumishi wa TSC wana wajibu mkubwa kuhakikisha kero na malalamiko ya walimu yanafanyiwa kazi kwa wakati ili walimu nao waweze kutoa huduma bora ya kufundisha wanafunzi. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa tumetimiza lengo la Waziri Mchengerwa pamoja na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuhakikisha Serikali inamaliza kero na malalamiko ya walimu wote nchini.

BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti**
Paulina M. Nkwama


**Wajumbe**
Richard L. Odongo
Revocatus P. Misonge
Mectildis F. Kapinga
Lameck S. Mbeya
Zachary A. Dida
Fatuma I. Muya

**Mhariri Mkuu**
Gerard J. Chami

**Mhariri**
Adili J. Mhina

**Msanifu Kurasa**
Lucas G. Ogunde

## KATUNI



# WAZIRI MCHENGERWA AWAONYA WATENDAJI WASIOWAJIBIKA, AAHIDI KUIREJESHA TAMISEMI KWA WANANCHI

**Na Mwandishi wetu – Dodoma.**

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Mohamed Mchengerwa amewaonya watendaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ambao ni wabadhilifu, wala rushwa na wasiowajibika katika utendaji kazi wao hawatakuwa sehemu ya utendaji kazi wake.

Alisema atairejesha wizara hiyo kwa wananchi kwa kuhakikisha viongozi wote wanasikiliza na kutatua kero zao kwa wakati.

Mchengerwa aliyasema hayo Septemba 4, 2023 Jijini Dodoma mara baada ya kuwasili katika Ofisi za TAMISEMI zilizopo Mji wa Serikali, Mtumba.

"Niwaombe watumishi wenzangu kuwa sasa tunairejesha Ofisi ya Rais-TAMISEMI kwa wananchi, maana yake tunataka kufanya kazi hasa, ili tuweze kufanikiwa na malengo ya Mhe. Rais yaweze kutimia. Hivyo lazima tufanye kazi usiku na mchana hakuna namna. Wizara yetu tunaisogeza kwa wananchi, tutasikiliza kero za wananchi," amesema Mhe. Mchengerwa.

Aidha, alitumia fursa hiyo kuwaagiza wakuu wa mikoa na wilaya kuhakikisha wanatoka ofisini na kwenda kusikiliza na kutatua kero za wananchi na kusisitiza kuwa asilimia 45 ya wakuu wa wilaya hawafanyi majukumu yao.

"Kuanzia sasa wakuu wa mikoa wote, wakuu wa wilaya washuke chini kusikiliza kero za wananchi, asilimia 45 ya wakuu wa wilaya hawafanyi kazi kabisa, hawasikilizi kero za wananchi, kwa hiyo tunataka kila mmoja afanye kazi ili tuweze kutimiza malengo ya Watanzania, malengo ya Chama cha Mapinduzi, na malengo ya Rais wetu," amesisitiza Mhe. Mchengerwa.

Kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Mchengerwa aliwaonya wakurugenzi wa halmashauri ambao wamekalia fedha za miradi na kusisitiza kuwa hataongeza muda wa utekelezaji wa miradi hiyo.

"Mhe. Waziri Kairuki umesema kuna miradi mingi ambayo tayari imeshaanzwa lakini kuna baadhi ya watu hawajaitimiza, uliwawekea deadline, sitaongeza hata siku moja, na nitaomba unikabidhi hayo makaratasi, kila mmoja kule aliko lazima ajue, Wakurugenzi ambao wamekalia fedha za miradi sitaongeza siku hata moja," amefafanua Mhe. Mchengerwa.



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Mohamed Mchengerwa (Mb) akipokea taarifa ya makabidhiano na vitendea kazi kutoka kwa aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mhe. Angellah Kairuki ambaye kwa sasa ni Waziri Maliasili na Utalii, mara baada ya kuwasili Ofisi za Wizara zilizopo Mji wa Kiserikali Mtumba jijini Dodoma na kupokelewa na watumishi wakiwemo Viongozi, tarehe 04 Septemba, 2023.*



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Mohamed Mchengerwa (Mb) akikabidhi tuzo kwa aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mhe. Angellah Kairuki ambaye sasa ni Waziri Maliasili na Utalii kwa kutambua mchango wa utumishi wake katika Ofisi ya Rais TAMISEMI, tarehe 04 Septemba, 2023. Makabidhiano hayo yalifanyika katika Ofisi za Wizara zilipo Mji wa Kiserikali, Mtumba jijini Dodoma.*



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Mohamed Mchengerwa (Mb) akisalimiana na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama mara baada ya kuwasili Ofisi za Wizara zilizopo Mji wa Kiserikali Mtumba jijini Dodoma tarehe 04 Septemba, 2023.*



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Mohamed Mchengerwa (Mb) (mwenye tai nyekundu) akiwa katika picha ya pamoja na Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Angellah Jasmine Kairuki (Mb) (wa tano kutoka kulia) pamoja na Viongozi na Menejimenti ya TAMISEMI wakati wa hafla ya kumkaribisha Waziri Mchengerwa katika Ofisi ya Rais TAMISEMI Septemba 4, 2023 jijini Dodoma.*



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Mohamed Mchengerwa (Mb) akiwa katika kikao cha ndani na Wajumbe wa Menejimenti ya TAMISEMI Septemba 4, 2023 jijini Dodoma.*



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Mohamed Mchengerwa (Mb) (mwenye tai nyekundu) akiwa katika picha ya pamoja na Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Angellah Jasmine Kairuki (Mb) (wa tatu kutoka kulia) pamoja na Viongozi na Menejimenti ya TAMISEMI wakati wa hafla ya kukaribisha Waziri Mchengerwa katika Ofisi ya Rais TAMISEMI Septemba 4, 2023 jijini Dodoma.*

*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akisalimiana na Naibu Waziri Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Dkt. Festo Dugange (Mb) wakati wa hafla ya kumpokea Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mhe. Mohamed Mchengerwa (Mb) Septemba 4, 2023 jijini Dodoma.*





*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akiongea na viongozi mbalimbali wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) wakati wa hafla ya kumpokea Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mhe. Mohamed Mchengerwa (Mb) Septemba 4, 2023 jijini Dodoma.*

# TSC YAWASILISHA TAARIFA YA AWALI KUHUSU MTIRIRIKO WA UPANDAJI VYEO KWA WALIMU KATIKA KUNDI RIKA

**Na Mwandishi wetu– Dodoma.**

Naibu Katibu Mkuu (Elimu) kutoka Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Dkt. Charles Msonde, Septemba 05, 2023 amekutana na Menejimenti ya Ofisi ya Rais - Tume ya Utumishi wa Walimu (OR-TSC) Jijini Dodoma katika Ukumbi wa Mikutano wa Tume hiyo ambapo Tume iliwasilisha Uchambuzi wa Taarifa kuhusu Mtiririko wa Upandaji Vyeo kwa Walimu katika Kundi Rika ikiwa ni pamoja na kupokea hatua iliyofikiwa ya ukamilishaji wa maoni na marekebisho ya Fomu ya Walimu Kuwasilisha Taarifa za Kiutumishi. Kikao hicho kiliongozwa na Naibu Katibu Mkuu huyo ambapo pia Katibu wa Tume hiyo, Mwl. Paulina M. Nkwama, *ndc* aliwaongoza Wajumbe wake wa Menejimenti.



*Naibu Katibu Mkuu (Elimu) kutoka Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Dkt. Charles Msonde akuzungumza na Wajumbe wa Menenjineti ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) (hawapo pichani) wakati TSC ikiwasilisha Uchambuzi wa Taarifa kuhusu Mtiririko wa Upandaji Vyeo kwa Walimu katika Kundi Rika Septemba 05, 2023 katika Ukumbi wa TSC Makao Makuu Dodoma.*



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akitoa ufafanuzi wa Uchambuzi wa Taarifa kuhusu Mtiririko wa Upandaji Vyeo kwa Walimu katika Kundi Rika kwa Naibu Katibu Mkuu (Elimu) kutoka Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Dkt. Charles Msonde (hayupo pichani) Septemba 05, 2023 katika Ukumbi wa TSC Makao Makuu Dodoma.*



*Kikao kati ya Naibu Katibu Mkuu (Elimu) kutoka Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Dkt. Charles Msonde na Menenjineti ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kikiwa kinaendelea.*



*Kikao kati ya Naibu Katibu Mkuu (Elimu) kutoka Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Dkt. Charles Msonde na Menenjineti ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kikiwa kinaendelea.*

# MASHAURI YA KOSA LA UTORO KAZINI KWA WALIMU WILAYANI LONGIDO YAWA SUGU

- Vitabu 122 vya Ufafanuzi wa Kanuni kwa Walimu vyagawiwa;
- Shule 63 zikiwemo za Msingi na Sekondari zanufaika na elimu hiyo;
- Changamoto kubwa ya wanafunzi kuacha masomo yabainika; na
- Mila na desturi za jamii za kifugaji zabainika chanzo uachaji masomo.

**Na. Mwandishi Wetu – Longido.**

Mashauri ya Kosa la Utoro Kazini kwa Walimu Wilayani Longido yamebainika kuwa sugu huku ikielezwa kuwa sababu kubwa ni mazingira magumu ya kazi kwa nyanja ya malazi na makazi kwani wengi wanashindwa kuishi kwenye maboma ambayo ndiyo sehemu kubwa ya malazi na makazi ya Wananchi wa Wilayani humo.

Hilo limeelezwa hivi karibuni na Kaimu Katibu Msaidizi wa Ofisi ya TSC Wilayani Longido, Mwl. Tumaini Chugala, katika taarifa yake iliyowasilishwa kwa Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali, Ofisi ya Rais – TSC Makao Makuu, Ndg. Gerard Chami, akiwa katika ziara za kila mwezi kupata habari za utekelezaji wa majukumu ya Tume hiyo katika Ofisi za Wilaya.

"Katika hii Wilaya yetu ya Longido, nidhamu za Walimu katika kufuata Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali zinazoongoza Utumishi wa Walimu na Umma vimeendelea kuzingatiwa na Walimu walio wengi na hata wale wachache wanaovunja taratibu hizo, hatua mbalimbali za kinidhamu zimekua zikichukuliwa kwa wakati katika Mamlaka ya Nidhamu ngazi ya Shule na Wilaya na hivyo kufanya makosa hayo ya kinidhamu kutokuwa mengi lakini kwa sehemu kubwa mashauri ya utoro kazini yakijirudia." Taarifa hiyo ya Kaimu Katibu Msaidizi huyo wa Ofisi ya TSC Wilayani Longido ilisema.

Aidha, pamoja na usugu wa mashauri ya kosa hilo la utoro wa Walimu katika vituo vyao vya kazi wilayani humo alisema kumekua na changamoto kubwa ya wanafunzi walio wengi wilayani humo kuacha masomo inayowakabili hasa watoto wa Shule za Msingi kitu kinachosababishwa na mila na desturi za maeneo hayo ambayo kwa sehemu kubwa yamezingatia na kutoa kipaumbele katika eneo la ufugaji vile wilaya niya kifugaji zaidi.

Katika kukabiliana na changamoto hizo na hasa ile ya utoro wa Walimu, Kaimu Katibu huyo Msaidizi alisema jitihada za makusudi zinafanyika ikiwa ni pamoja na kugawa vitabu 122 kwa Walimu wa Shule zote za Msingi na Sekondari zipatazo 63 vyenye Ufafanuzi wa Kanuni za Utumishi na Utendaji Kazi wa Walimu zoezi linaloenda sambamba na uhamasishaji na utoaji elimu kwa Walimu kuhusiana na masuala mbalimbali ya Kiutumishi na Kiutendaji.



*Afisa wa TSC Wilaya ya Longido, Mwl. Boniphace Bita akiongea na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali wa TSC Makao Makuu, Gerard Chami (hayupo pichani) wakati wa ziara ya Mkuu huyo wa Kitengo aliyoifanya Wilayani Longido hivi karibuni.*



*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali wa TSC Makao Makuu, Gerard Chami akizungumza wakati wa kikao chake na Afisa wa TSC Wilaya ya Longido, Mwl. Boniphace Bita kilichofanyika katika ofisi za TSC Longido hivi karibuni*



*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali wa TSC Makao Makuu, Gerard Chami akipitia nyaraka wakati wa wakati wa kikao chake na Afisa wa TSC Wilaya ya Longido, Mwl. Boniphace Bita kilichofanyika katika ofisi za TSC Longido hivi karibuni.*

# TSC MULEBA YATOA MAFUNZO KWA WALIMU 144 WA AJIRA MPYA

**Na Mwandishi wetu – Muleba.**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Muleba kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo imeendesha mafunzo kwa walimu 144 wa ajira mpya kwa lengo la kuwajengea uelewa juu ya Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Walimu.

Katika mafunzo hayo, walimu walifundishwa juu ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji kazi katika Utumishi wa Walimu, Haki na Wajibu wa Mwalimu, aina za Makosa ya Nidhamu katika Utumishi wa Walimu na Adhabu zake pamoja na Maandalizi ya Ufundishaji na Ujifunzaji.





Katika Ajira za Ualimu zilizotolewa na Serikali na Walimu kupangiwa vituo vya kazi mwezi Juni, 2023 Wilaya ya Muleba ilipangiwa walimu 148 ambapo walimu 144 ndiyo walioripoti kazini.

















# WALIMU 730 KUTOKA SHULE 57 NDANI YA KATA SABA WILAYANI KARATU WAFIKIWA NA ELIMU YA UFAFANUZI WA KANUNI ZA MAADILI NA UTENDAJI KAZI KATIKA UTUMISHI - TSC KARATU

- **Lengo ni kufikia Walimu wote 1,599 kutoka Shule zote 146;**
- **Vitabu 101 kati ya 127 vya Ufafanuzi wa Kanuni wagawiwa Walimu;**
- **Hali ya nidhamu za Walimu yazidi kuimarika;**
- **Idadi ya makosa na mashauri ya Walimu yazidi kuporomoka;**
- **Shule za Sekondari zaendelea kupata mashauri zaidi ya utoro;**
- **Walimu 58 wa Ajira Mpya kati yao 33 wa Sayansi wapangiwa Shule;**
- **Waajiri waombwa kuizingatia Sheria ya TSC.**





*Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Karatu, Mwl. Stephano Mosha akiongea katika kikao na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali wa TSC Makao Makuu, Gerard Chami wakati wa ziara ya Mkuu huyo wa Kitengo aliyoifanya Wilayani Karatu hivi karibuni.*

**Na. Mwandishi Wetu – Karatu.**

Ofisi ya Rais – Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilayani Karatu Mkoani Arusha imefanikiwa kuwafikia Walimu 730 wa Shule za Msingi (413) na Sekondari (317) kutoka Shule 57; Msingi (42) na Sekondari (15) kati ya 146 zilizopo Wilayani humo ndani ya Kata saba kati ya 22 ili kuwahamasisha na kuwajengea uelewa zaidi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu ikiwa ni moja ya utekelezaji wa ufafanuzi wa kanuni hizo kwa Walimu.

Hilo limebainika hivi karibuni wakati Kaimu Katibu Msaidizi wa Ofisi ya TSC Wilayani Karatu, Ndg. Stephano Mosha, alipokuwa akiongea na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali, Ofisi ya Rais – TSC Makao Makuu, Ndg. Gerard Chami, akiwa katika ziara za kila mwezi kupata habari za utekelezaji wa majukumu ya Tume hiyo katika Ofisi za Wilaya na zaidi juu ya utekelezaji wa zoezi la uhamasishaji, kujengeana uwezo kwa utoaji elimu ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu kwa Walimu Wilayani humo.

"Pamoja na Walimu wa Shule hizo tulizofanikiwa kuzifikia mpaka sasa, tumefanikiwa pia kutoa elimu na kuongea na Walimu juu ya changamoto zao mbalimbali ambazo zinawakabili nakwa pamoja kujitahidi kuzitafutia ufumbuzi na ushauri ikiwa ni pamoja na kuwakabidhi vitabu 101 kati ya 127 vilivyopokelewa vya Ufafanuzi wa Kanuni hizo kutoka Makao Makuu kwa rejea yao kiutendaji." Alisema

# WALIMU 730 KUTOKA SHULE 57 NDANI YA KATA SABA WILAYANI KARATU WAFIKIWA NA ELIMU YA UFAFANUZI WA KANUNI ZA MAADILI NA UTENDAJI KAZI KATIKA UTUMISHI - TSC KARATU

Kaimu Katibu Msaidizi huyo wa Ofisi ya TSC Wilayani Karatu.

Ndg. Mosha alisema mikakati ya kuwatembelea Walimu zaidi katika vituo vyao vya kazi wilayani humo inaendelea kufanyiwa kazi ili kuitekeleza kama ratiba ya ziara hizo ilivyopangwa kwani mara nyingi imekua ikiathiriwa na mwingiliano wa shughuli nyingine za huduma kwa Walimu na zile za Kitaifa ikiwemo mazoezi maalumu ya upandishaji vyeo, utekelezaji wa viashiria vya utendaji (KPIs) na Mitihani ya Darasa la Saba.



*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali wa TSC Makao Makuu, Gerard Chami akipitia nyaraka wakati wa kikao chake na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Karatu, Mwl. Stephano Mosha kilichofanyika hivi karibuni.*

Aidha, Kaimu Katibu Msaidizi huyo alisema kutokana na mwendelezo wa utoaji elimu na ugawaji wa vitabu vya ufafanuzi wa kanuni za maadili na utendaji kazi katika utumishi wa walimu hali ya nidhamu ya walimu imeendelea kuimarika na kusababisha kupungua kwa idadi ya aina ya makosa na idadi ya mashauri ya Walimu ambayo tangu kuanza kwa utekelezaji wa robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2023/ 2024 jumla ya mashauri matatu tu ndiyo yamepokelewa yote kutoka shule za sekondari na yote yakiwa ya utoro tofauti na siku za nyuma.

Kadhalika, Ndg.Mosha alitumia fursa hiyo kuishukuru Serikali, Wizara Mama na Tume ya Utumishi wa Walimu Makao Makuu kwa kufanikisha Wilaya ya Karatu kupangiwa Walimu wa Ajira Mpya 58 ambapo kati yao Walimu 23 walipangiwa Shule za Msingi na Walimu 35; ambao kati yao Walimu 33 ni Walimu wa Sayansi na Walimu wawili 'Arts' walipangiwa Shule za Sekondari na hivyo kuiimarisha zaidi Wilaya hiyo katika eneo la Masomo ya Sayansi.



*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali wa TSC Makao Makuu, Gerard Chami akizungumza wakati wa kikao chake na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Karatu, Mwl. Stephano Mosha kilichofanyika hivi karibuni.*

Vilevile Kaimu Katibu huyo Msaidizi aliendelea kuwasihi Waajiri wote nchini kuendelea kuizingatia Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu kwa kuzipa nafasi Kamati za Wilaya katika kufanya uchunguzi wa mashauri mbalimbali ya Walimu na kufanya vikao vya maamuzi badala ya wao kuchukua hatua ya hukumu kwa Mwalimu kinyume na Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo iliyopo katika Utumishi wa Walimu.

Ofisi ya TSC Wilayani Karatu inahudumia jumla ya Walimu 1,599; ambapo 948 ni Walimu wa Shule za Msingi na 651 ni Walimu wa Shule za Sekondari huku ikihudumu katika jumla ya shule 154; ambapo 113 ni Shule za Msingi, 33 za Sekondari na Shikizi nane (sita zikiwa zimepokea wanafunzi na kuanza kufundisha huku mbili zikiwa zinasubiri mchakato wa kuhamishiwa wanafunzi).

# WALIMU 51 AJIRA MPYA WILAYANI LONGIDO WAFANYIWA USAJILI KUPITIA TSCMIS

**Na Mwandishi wetu – Longido.**

**"Kuhusiana na Mfumo wa TSCMIS, Tume ngazi ya Wilaya imeweza kuutumia katika usajili wa walimu wa ajira mpya ya Juni, 2023 ambapo jumla ya walimu 51 wamesajiliwa na kupewa barua za ajira pamoja na mikataba. Katika idadi hiyo walimu 40 ni wa shule za msingi na 11 ni wa shule za sekondari."**

Katika kutekeleza maelelezo yaliyotolewa na Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Makao Makuu kwa Ofisi zote za Tume ngazi ya Wilaya la kusajili wa walimu wa ajira mpya kupitia mfumo wa Teachers' Srvice Commission Management Information System (TSCMIS), TSC Wilaya ya Longido imetekeleza agizo hilo kikamilifu ambapo jumla ya walimu 51 wamesajiliwa kupitia mfumo huo.

Hayo yameelezwa hivi karibuni na Kaimu Katibu MSaidizi wa TSC Wilaya ya Longido, Tumaini Chugala wakati Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali, Gerard Chami alipofanya ziara ofisini hapo kwa lengo la kuona namna utekelezaji wa Majukumu ya Tume yanavyotekelezwa katika ofisi hiyo.

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa majukumu hayo, kwa niaba ya Kaimu Katibu Msaidizi huyo, Mwl. Boniphace Bita alieleza kuwa kazi ya usajili wa walimu katika mfumo wa TSCMIS imefanyika kwa ufanisi na kutokana na kuwepo kwa ushirikiano wa karibu kati ya ofisi hiyo na maafisa wa TEHAMA kutoka TSC Makao Makuu.

Mfumo wa TSCMIS unajumuisha moduli sita (6) ambazo ni; Disciplinary (Mashauri ya Nidhamu), Appeal (Rufaa), Gratuity and Pension Computation (Mafao na Pession), Complaints (Malalamiko), Registration (Usajili) pamoja na Visitors and Helpdesk (Wageni na dawati la usaidizi).

Hivyo, zoezi la usajili wa walimu kupitia mfumo huo ni matumizi ya moduli moja (1) kati ya sita (6) zilizokusudiwa kutumika katika kutoa huduma kwa walimu, hivyo Mwl. Chugala aliomba Ofisi ya TSC Longido kupatiwa mafunzo ya matumizi ya moduli zingine ili kuweza kuongeza wigo wa kutoa huduma kwa walengwa.

"Kutokana na kwamba mfumo huu bado ni mpya lakini pia ofisi yetu haikupata mafunzo rasmi ya matumizi ya mfumo huu, tunaomba kupewa mafunzo ili tuweze kuwa mahiri katika kutumia moduli zote sita (6) ili tuweze kuongeza ubora katika kutoa huduma kwa walimu wetu," alieza Mwl. Chugala katika taarifa yake iliyowasilishwa na Mwl. Bita.

Hivi karibuni Katibu wa TSC, MWl. Paulina Nkwama alikaririwa na vyombo vya habari akizungumzia faida mbalimbali za mfumo wa TSCMIS ambapo alisema utarahisisha na kuboresha utendaji kazi wa shughuli za kila siku katika kuwahudumia walimu kwenye masuala ya ajira (usajili na kuthibitishwa kazini), maendeleo ya Walimu (kupandishwa vyeo na kubadilishiwa muundo wa utumishi), mafao, mashauri ya nidhamu pamoja na rufaa za walimu.

Pia, alieleza kuwa, matumizi ya mfumo yataongeza ufanisi katika kushughulikia Utumishi wa Walimu na utamfanya mwalimu asihangaike kutafuta huduma. Kama atakuwa na hoja zake ataingia kwenye mfumo atatoa taarifa ataweka hoja yake atatuma. Akishatuma ana uwezo wa kufuatilia na kuona hoja yake ilipofikia na pale itakapokuwa imejibiwa atapata majibu hapo hapo. Hivyo, kwa kupitia simu ya mkononi mwalimu atapata huduma zote za kiutumishi.

Kwa mujibu wa Mwl. Nkwama, Mfumo wa TSCMIS utasaidia kuondoa changamoto za upatikanaji wa taarifa kwa wakati hususan taarifa za wilaya. Mfumo huo una uwezo wa kutunza na kutoa taarifa ya kila kinachofanyika kuanzia ngazi ya shule hadi TSC Makao Makuu.



*Afisa wa TSC Wilaya ya Longido, Mwl. Boniphace Bita akiongeza na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali wa TSC Makao Makuu, Gerard Chami wakati wa ziara ya Mkuu huyo wa Kitengo aliyoifanya Wilayani Longido hivi karibuni.*



*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali wa TSC, Gerard Chami akizungumza wakati wa kikao chake na Afisa wa TSC wa Wilaya ya Longido, Mwl. Boniphace Bita kilichofanyika katika ofisi za TSC Longido hivi karibuni.*




*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akiwa katika mahojiano na Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) ambapo alizungumzia faida mbalimbali za Mfumo wa Teachers' Service Commission Management Information System (TSCMIS).*



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akuzungumza katika kikao cha awali cha Menejimenti ya TSC na Wakaguzi wa Nje wa Hesabu za Serikali kutoka Ofisi ya Taifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kikilenga kuanza kwa ukaguzi wa hesabu za Tume kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Kikao hicho kilifanyika hivi karibuni katika ofisi za TSC Makao Makuu Dodoma.*



*Mmoja wa Maafisa kutoka kutoka Ofisi ya Taifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali akuzungumza katika kikao cha awali cha Menejimenti ya TSC na Wakaguzi wa Nje wa Hesabu za Serikali kilicholenga kuanza kwa ukaguzi wa hesabu za TSC kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Kikao hicho kilifanyika hivi karibuni katika ofisi za TSC Makao Makuu Dodoma.*







*Kikao cha awali cha Menejimenti ya TSC na Wakaguzi wa Nje wa Hesabu za Serikali kilicholenga kuanza kwa ukaguzi wa hesabu za TSC kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kikiwa kinaendelea. Kikao hicho kilifanyika hivi karibuni katika ofisi za TSC Makao Makuu Dodoma.*

# TSC MONDULI YABAINISHA USHIRIKIANO BAINA YA HALMASHAURI NA OFISI ZA TSC WILAYA KUWA CHACHU KUBWA YA UELIMISHAJI WALIMU JUU YA MASUALA YA KIUTUMISHI NA KIUTENDAJI KAZINI

**Na. Mwandishi Wetu – Monduli.**

Ushirikiano mkubwa baina na Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Monduli Mkoani Arusha, Wadau mbalimbali na Ofisi ya Wilaya ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilayani Monduli, umebainika kuwa chachu baada ya sehemu kubwa ya matukio na mihadhara mbalimbali ya Halmashauri na Wadau hao kutumika kutoa elimu na kujengeana uwezo katika masuala mbalimbali ya Utumishi na Utendaji Kazi wa Walimu hao.

Hilo limebainika hivi karibuni wakati Kaimu Katibu Msaidizi wa Ofisi ya TSC Wilayani Monduli, Mwl. Joyce Macha, alipokua akiongea na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali, Ofisi ya Rais – TSC Makao Makuu, Ndg. Gerard Chami, akiwa katika ziara za kila mwezi kupata habari za utekelezaji wa majukumu ya Tume hiyo katika Ofisi za Wilaya.

"Kwakweli Mkurugenzi wa Halmashauri pamoja na Wadau mbalimbali wakiwemo Chama cha Walimu Tanzania (CWT, MEWAKA na wengineo; wamekua wakitupa ushirikiano wa karibu sana kwa kutualika na kutushirikisha katika matukio na mihadhara mbalimbali ya Halmashauri na Wadau hao na tumekua kwa pamoja tukitoa elimu na kuwajengea Walimu wetu uwezo katika masuala mbalimbali ya Utumishi na Utendaji wao wa Kazi na zaidi ni juu ya zoezi la uhamasishaji na utoaji elimu ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu hapa wilayani." Alisema Kaimu Katibu Msaidizi huyo wa Ofisi ya TSC Wilayani Monduli.

Mwl.Macha alisema tangu kuanza kwa utekelezaji wa zoezi la utoaji elimu na uhamasishaji Walimu juu ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu wamezifikia kwa vipindi tofauti Shule za Msingi na Sekondari katika Kata sita kati ya 20 ambazo zina jumla ya Shule za Serikali 79 ikiwa za Msingi ni 65 na Sekondari 14 zinazohudumiwa na Walimu 1,070 ambapo kati yao wa Msingi ni 681 (Wanawake 410 na Wanaume 271) na Serkondari 389 (Wanawake 150 na Wanaume



*Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Monduli, Mwl. Joyce Macha akiongea katika kikao cha watumishi wa ofisi hiyo na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali wa TSC, Gerard Chami wakati wa ziara ya Mkuu huyo wa Kitengo aliyoifanya Wilayani Monduli hivi karibuni.*

# TSC MONDULI YABAINISHA USHIRIKIANO BAINA YA HALMASHAURI NA OFISI ZA TSC WILAYA KUWA CHACHU KUBWA YA UELIMISHAJI WALIMU JUU YA MASUALA YA KIUTUMISHI NA KIUTENDAJI KAZINI

239).

Aidha, Kaimu Katibu huyo Msaidizi alitoa pongezi kwa Serikali kupitia Ofisi ya TSC Makao Makuu kwa uhamasishaji wa ujenzi na matumizi ya mifumo ya TEHAMA ambayo alisema kwa kiwango kikubwa imerahisisha sana utendaji kazi kwa wakati na kuepuka matumizi makubwa ya shajara za ofisi akitolea mfano usajili wa Walimu wapya 13 waliopangiwa Wilayani Monduli ambao wote walisajiliwa kupitia Mfumo wa Kielektroniki wa Tume ya Utumishi wa Walimu ujulikanao kama TSCMIS.

Vilevile Mwl. Macha akiongelea eneo la upandishaji vyeo na ubadilishaji kazi Walimu alisema, Ofisi yake Wilayani humo ilifanikliwa kuwapandisha vyeo na kuhakikisha wamebadilishiwa mishahara yao jumla ya Walimu 389 ambao kati ya hao; Walimu 301 walikuwa wa Shule za Msingi huku 88 wakiwa wa Sekondari na Walimu nane walibadilishiwa kazi kama walivyoomba baada ya kujiendeleza kitaaluma.



*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali wa TSC Makao Makuu, Gerard Chami (wa pili kutoka kulia) akiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa TSC Wilaya ya Monduli wakati wa ziara yake aliyoifanya wilayani hapo hivi karibuni.*

Akimalizia kwa kuzungumzia hali ya nidhamu kwa Walimu ndani ya Wilaya hiyo Kaimu Katibu Msaidizi huyo Mwl. Macha alisema hali ya nidhamu niya kuridhisha kwani kwa kipindi cha Mwaka 2022/2023 Ofisi yake ilipokea jumla ya Mashauri ya Nidhamu ya Walimu 10 ambayo ni sawa na asilimia 0.93 ikilinganishwa na miaka ya nyuma.

Alisema hali hiyo inachangiwa na Wakuu wa Shule na Walimu Wakuu kutekeleza majukumu yao kwa Mujibu wa Sheria ya Tume kwani wamekuwa wakimaliza baadhi ya mashauri ya makosa madogo-madogo yanayoruhusiwa kumalizika shuleni.

Ofisi ya TSC Wilayani Monduli ni miongoni mwa Ofisi sita zilizopo Mkoani Arusha. Wilaya hii kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 ina jumla ya Watu 227,585 ikiwa ni Wanawake 12,843 na Wanaume 104,742 na ikipakana na Wilaya ya Longido kwa upande wa Kaskazini, Wilaya ya Arumeru kwa upande Mashariki, Wilaya ya Simanjiro kwa upande wa Kusini nakwa upande wa Magharibi inapakana na Wilaya ya Babati.



*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali wa TSC Makao Makuu, Gerard Chami akizungumza wakati wa kikao chake na watumishi wa TSC Wilaya ya Monduli kilichofanyika hivi karibuni.*

# TUME YA UTUMISHI WA WALIMU CHAGIZO LA UFAULU ARUSHA JIJI

- Jiji lashika nafasi ya kwanza kimkoa miaka mitatu mfululizo;
- Maelekezo ya Serikali huduma vituoni kwa Walimu yatekelezwa;
- Huduma kwa Walimu, mara tatu kwa wiki mashuleni; na
- TSCMIS yaleta tija Usajili na Utoaji Mikataba ya Ajira kwa Walimu.

**Na. Mwandishi Wetu – Arusha.**

Utekelezaji wa jukumu la usimamizi mzuri wa eneo la nidhamu na maadili ya Walimu chini ya Ofisi ya Rais – Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), umepelekea utendaji mzuri wenye weledi na tija kwa Taifa kwa Walimu walio wengi Jijini Arusha hali iliyopelekea Halmashauri ya Jiji hilo kwa upande wa Elimu ya Msingi kushika nafasi ya kwanza kimkoa kwa miaka mitatu mfululizo katika matokeo ya Darasa la Saba.

Hilo limebainika hivi karibuni wakati Kaimu Katibu Msaidizi wa Ofisi ya TSC Jijini Arusha, Ndg. Gerald Iron William, alipokuwa akiongea na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka Ofisi ya Rais – TSC Makao Makuu, Ndg. Gerard Chami, akiwa katika ziara yake ya ufuatiliaji habari mbalimbali za utekelezaji wa majukumu ya Tume hiyo katika Ofisi za Wilaya na utekelezaji wa zoezi la uhamasishaji na utoaji elimu kwa Walimu juu ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu Jijini humo.

"Tunasimamia na kutekeleza vema jukumu letu la Kisheria katika kuhakikisha Walimu wanaepukana na makosa mbalimbali madogo kwa makubwa kwa namna mbalimbali lakini kubwa ikiwa ni kuendelea kuwapa elimu kila siku kwa njia na namna mbalimbali. Jambo hili limetusaidia sana sisi kupunguza mashauri lakini pia limeleta matokeo chanya katika utendaji kazi mzuri wa Walimu wetu ambao wameimarika kinidhamu hali iliyopelekea halmashauri ya Jiji letu la Arusha kwa upande wa Elimu Msingi kushika nafasi ya kwanza kimkoa kwa matokeo ya darasa la saba kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo." Alisema Kaimu Katibu Msaidizi huyo wa Ofisi ya TSC Jijini Arusha.

Ndg. William alisema katika kuendelea kuliimarisha zaidi eneo hilo la nidhamu na maadili Pamoja na maeneo mengine yanayosimamiwa na Tume, wamejiwekea mkakati endelevu wa kutembelea Walimu mara tatu kwa wiki katika vituo vyao vyote vya kazi (shuleni) vinavyosimamiwa na Ofisi ya TSC Jijini hapo ili kutoa huduma badala ya Mwalimu kuacha majukumu ya kumlea



*Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Arusha, Gerald William akiongeza katika kikao cha watumishi wa ofisi hiyo na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali wa TSC Makao Makuu, Gerard Chami (hawapo pichani) wakati wa ziara ya Mkuu huyo wa Kitengo aliyoifanya Wilayani Arusha hivi karibuni.*



*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali wa TSC Makao Makuu, Gerard Chami akizungumza wakatia wa kikao chake na watumishi wa TSC Wilaya ya Arusha kilichofanyika hivi karibuni.*

# TUME YA UTUMISHI WA WALIMU CHAGIZO LA UFAULU ARUSHA JIJI

na kumfundisha mwanafunzi na kufuata huduma za kiutumishi zilipo Ofisi za TSC jambo ambalo alikiri kuwa tayari shule 17 (Msingi 11 na sita za Sekondari) kati ya 80 (Msingi 49 na 31 za Sekondari) za Jijini hapo zimeshatembelewa na kupewa huduma hizo ikiwemo elimu ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Ualimu.

Aidha, Kaimu Katibu Msaidizi huyo alisema kutokana na mwendelezo wa utoaji elimu na ugawaji wa vitabu vya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu, jumla ya Walimu 2,617 wanaohudumiwa na ofisi yake wanatarajiwa kufikiwa ambapo kati yao Walimu wa Msingi ni 1,528 (Wanawake 1,301 na 227 Wanaume) huku Sekondari matarajio yakiwa ni Walimu 1,089 (Wanawake 679 na 410 Wanaume) ambao kwa ujumla wao wanatoa elimu kwa Wanafunzi 110,841 ikiwa ni Msingi 79,738 (Wasichana 40,128 na 39,610 Wavulana) na Sekondari 31,103 (Wasichana 16,064 na 15,039 Wavulana).

Kadhalika, Ndg.William alitumia fursa hiyo kusema kuwa utekelezaji wa utoaji huduma kwa Walimu kwa kuwafikia vituoni mwao kwa vitendo ni utekelezaji wa maelekezo ya Serikali kupitia Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Ofisi ya TSC Makao Makuu chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Tume, Mwl. Paulina Mbena Nkwama, ndc.

Vilevile Kaimu Katibu huyo Msaidizi alisema Ofisi yake imeendelea kupokea barua za maombi ya Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari kuomba kubadilishiwa vyeo na kazi baada ya kujiendeleza kitaaluma na kupokea Walimu wapya wa Sekondari ambazo ni juhudi na jitihada za Serikali katika kuiimarisha zaidi Sekta ya Elimu Jijini Arusha na nchini kwa ujumla.

Akiongezea katika hilo Ndg. William alisema Ofisi ya TSC Jijini Arusha kwa kushirikiana na Halmashauri ya Jiji la Arusha katika Mwaka wa Fedha 2022/ 2023 walifanikiwa kuwapandisha vyeo/ madaraja jumla ya Walimu 1,023 ambapo kati ya hao Walimu 653 (Wanawake 574 na 79 Wanaume) walikuwa wa Shule za Msingi na 370 (Wanawake 248 na 122 Wanaume) walikuwa wa Shule za Sekondari.

Vilevile alisema Ofisi yake imetoa vibali sita vya kustaafu ambapo kimoja nicha Mwalimu wa Shule ya Sekondari na vitano vya Walimu wa Shule za Msingi huku Mfumo wa Tume wa Kielektroniki ujulikanao kama TSCMIS ukitumika vema kusajili Walimu wa ajira mpya na kutoa namba zao za usajili kwa urahisi na haraka zaidi tofauti na uendeshaji zoezi la usajili ulivyokua ukifanyika hapo awali kwa njia ya majalada magumu.

Halmashauri ya Jiji la Arusha ina jumla ya Shule Shikizi nne ambazo ziko katika hatua ya ujenzi kati ya hizo tatu zikiwa ni Shule za Msingi na moja ya Sekondari.



*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali wa TSC Makao Makuu, Gerard Chami pamoja na watumishi wa TSC Wilaya ya Arusha wakipitia baadhi ya nyaraka wakati wa ziara ya Mkuu huyo wa Kitengo aliyoifanya Wilayani Arusha hivi karibuni.*



*Watumishi wa TSC Wilaya ya Arusha wakiwa katika kikao na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali wa TSC Makao Makuu, Gerard Chami kilichofanyika hivi karibuni katika Ofisi za TSC Wilaya ya Arusha.*

# TSC ARUMERU YAENDELEA KUTOA ELIMU KUHUSU UFAFANUZI WA MAADILI NA UTENDAJI KAZI KATIKA UTUMISHI WA WALIMU

**Na Mwandishi wetu – Arumeru.**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Arumeru imeendelea kutoa elimu kwa walimu kuhusu Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji kazi katika Utumishi wa Walimu kwa lengo la kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia Sheria Kanuni na Taratibu za utumishi huo.

Hayo yamebainishwa na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Arumeru, Bi Zeituni Kinkwerema wakati wa ziara ya Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali wa TSC, Gerard Chami aliyoifanya wilayani hapo hivi karibuni.



*Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Arumeru, Bi Zeituni Kinkwerema akiongeza katika kikao cha watumishi wa ofisi hiyo na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali wa TSC Makao Makuu, Gerard Chami (hawapo pichani) wakati wa ziara ya Mkuu huyo wa Kitengo aliyoifanya Wilayani Arumeru hivi karibuni.*

Alisema pamoja na kuwafikia walimu moja kwa moja kwa kufanya ziara shuleni, Ofisi hiyo ilifanikiwa kuanzisha jukwaa la utoaji elimu juu ya Ufafanuzi huo kwa fungua kundi la WhatsApp ambapo walimu wengi wamepata elimu kwa njia hiyo.

"Katika utekelezaji wa Utoaji Elimu kwa Walimu kuhusu ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji kazi katika Utumishi wa Walimu tuliweza kuwafikia Walimu na kuwaelimisha kwa kutengeneza kundi la Whatsapp ambalo tuliweka nakala laini ya kitabu cha Ufafanuzi wa kanuni za Utumishi wa Walimu. Walimu waliweza kupitia na kusoma maudhui yaliyoainishwa, pia walipata ufafaunuzi wa maswali mbalimbali yaliyokuwa yanawatatiza," alisema.

Aliendelea kufafanua kuwa, "pia tuliweza kufanya ziara na kuzifikia baadhi ya Shule moja moja na baadae kuandaa ratiba ya kuwafikia Walimu na kuwaelimisha kwa kata. Shule zilizofikiwa katika Halmashauri ya Meru ni Kikatiti na Chemchem kwa Shule za Msingi na kwa Shule za Sekondari ni Akeri na Nasholi."

Aidha, Kinkwerema alieleza kuwa kwa upande wa Halmashauri ya Wilaya ya Arusha ofisi yake ilitembelea Shule za Sekondari Mateves na Mringa, Pia utekelezaji umefanywa kwa kata katika kata ya Oldonyowasi yenye shule za Sekondari Namelok, Engutukoit, Losinoni Engedeko, Oldonyowasi na shule ya Msingi Oldonyowasi.

"Pia, katika kata ya Bwawani tulikutana na Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari za Themi ya Simba, Bwawani, Songambele, Kigongoni na Olokii."

Wilaya ya Arumeru ilipokea nakala za vitabu 120 vya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji kazi katika Utumishi wa Walimu kutoka TSC Makao Makuu kwa ajili ya kusambaza kwenye Halmashauri mbili ambavyo vililenga idara ya Elimu Msingi ambapo nakala 62 zimegawanywa katika Halmashauri ya Wilaya ya Meru na nakala 58 ziligawanya katika Halmashauri ya Arusha.

Akizungumzia changamoto zonazoikabidli ofisi hiyo, Kinkwerema alieleza kuwa kuna upungufu wa vitendea kazi hususan kompyuta, uchakavu wa vyumba vya ofisi, upungufu wa watumishi wa kuhudumia walimu wa halmashauri mbili, pomoja na kukosekana kwa uhakika wa vyombo vya usafiri kwa ajili ya kufanya ziara shuleni.

Kwa upande wake, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Gerard Chami alimpongeza Kaimu Katibu Msaidizi huyo kwa namna ofisi ya TSC Wilaya ya Arumeru inavyoendelea kutoa huduma kwa walimu huku akiahidi kuzifikisha changamoto zilizoibuliwa kwenye Menejimenti ya Tume kwa lengo la kupatiwa ufumbuzi.

Wilaya ya Arumeru ina jumla ya shule za Msingi 296 ambapo katika idadi hiyo Halmashauri ya Wilaya ya Meru in shule 116, na Halmashauri ya Wilaya ya Arusha ina Shule 100. Wilaya ya Arumeru ina Shule za Sekondari 80, Meru Shule 45, Halmashauri ya Arusha Shule 35.

Aidha, Wilaya ya Arumeru ina jumla ya walimu 5,135 ambapo katika idadi hiyo Walimu 2,563 ni wa Halmashauri ya Meru na 2,572 ni wa Halmashauri ya Arusha.



*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali wa TSC Makao Makuu, Gerard Chami (wa pili kutoka kushoto) akizungumza wakatia wa kikao chake na watumishi wa TSC Wilaya ya Arumeru kilichofanyika hivi karibuni.*



*Watumishi wa TSC Wilaya ya Arumeru wakiwa katika kikao na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali wa TSC Makao Makuu, Gerard Chami (hayupo pichani) kilichofanyika hivi karibuni katika Ofisi za TSC Wilaya ya Arumeru.*



*Mmoja wa watumishi wa TSC Wilaya ya Arumeru akichangia jambo wakati wa kikao cha watumishi hao na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali wa TSC Makao Makuu, Gerard Chami.*



*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali wa TSC Makao Makuu, Gerard Chami akikagua printa katika ofisi za TSC Wilaya ya Arumeru hivi karibuni.*

# WALIMU 291 WILAYANI LONGIDO WAPATIWA ELIMU JUU YA UFAFANUZI WA KANUNI ZA MAADILI NA UTENDAJI KAZI KATIKA UTUMISHI WA WALIMU

**Na. Mwandishi wetu – Longido.**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Longido imefanikiwa kuzifikia shule 21 za msingi na sekondari na kutoa elimu kwa walimu 291 kuhusu ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji kazi katika Utumishi wa Walimu kwa lengo kusaidia walimu wilayani hapo kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Walimu.

Hayo yamebainika katika taarifa ya Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Longido, Mwl. Tumaini Chugala iliyowasilishwa na Afisa wa TSC wa wilaya hiyo, Mwl. Boniphace Bita wakati wa ziara ya Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Gerard Chami iliyolenga kupata taarifa juu ya utekelezaji wa majukumu ya Tume katika wilaya hiyo.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa kabla ya kwenda kutoa elimu kwa walimu, Kamati ya TSC Wilaya ya Longido ilifanya kikazo kazi cha kupitia ufafanuzi huo kwa lengo la kupata uelewa wa pamoja na kisha wajumbe wa Kamati hiyo wakaamua njia madhubuti ya kufikisha elimu hiyo kwa walimu.

"Baada ya kupewa mafunzo na maelekezo kutoka TSC Makao Makuu ya kutoa elimu hii kwa walimu, sisi tulianza kutoa elimu kwa Wajumbe wa Kamati ambapo tulifanya kikao tarehe 14/03/2023. Baada ya hapo, Wajumbe hao walikubaliana kutafuta namna ya kufikisha elimu hiyo kwa walimu ambapo hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Agosti, 2023 tumefanikiwa kuzifikia shule 21," ilieleza sehemu ya taarifa hiyo.



*Afisa wa TSC Wilaya ya Longido, Mwl. Boniphace Bita akiongea na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali wa TSC Makao Makuu, Gerard Chami (hayupo pichani) wakati wa ziara ya Mkuu huyo wa Kitengo aliyoifanya Wilayani Longido hivi karibuni.*

Shule za Msingi zilizofikiwa katika utoaji wa elimu hiyo ni; Longido, Oltepes, Elerai, Irkaswa, Tingatinga, Orbomba, Kimokoua, Engarenaibor, Buguruni, Matale, Kitarini, Sokon, Lopolosek, Losirwa, Endirma na Gelairumbwa.

Kwa upande wa shule za Sekondari zilizofikiwa ni; Lekule, Matale, Namanga na Enduimet.

TSC Wilaya ya Longido kwa kushirikiana na wadau wengine ambao ni Ofisi ya Mkurugenzi, Chama cha Walimu na Ofisi ya Mthibiti Ubora wa Shule katika Wilaya hiyo inafanya juhudi kuhakikisha walimu wote wanafikiwa na kupatiwa elimu hiyo muhimu.

Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Longido inahudumia shule 63 ambapo kati ya hizo 54 ni za msingi na tisa (9) ni za Sekondari. Shule hizo zina jumla ya walimu 735, kati ya hao 460 ni wa shule za Msingi na 275 ni wa shule za Sekondari.



*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali wa TSC Makao Makuu, Gerard Chami akizungumza wakati wa kikao chake Afisa wa TSC Wilaya ya Longido, Mwl. Boniphace Bita kilichofanyika katika ofisi za TSC Longido hivi karibuni.*



*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali wa TSC Makao Makuu, Gerard Chami akipitia nyaraka wakati wa wakati wa kikao chake Afisa wa TSC Wilaya ya Longido, Mwl. Boniphace Bita kilichofanyika katika ofisi za TSC Longido hivi karibuni.*

# IJUE TSC WILAYA YA MONDULI NA NAMNA INAVYOTEKELEZA MAJUKUMU YAKE KATIKA KUHUDUMIA WALIMU

**Na Mwandishi wetu – Monduli.**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Monduli inahudumia jumla ya shule 79 ambapo shule za Msingi ni 65 na shule za sekondari ni 14 ambapo shule hizo zina jumla ya walimu 1070 kati ya hao walimu 681 ni wa shule za Msingi na walimu 389 ni wa shule za Sekondari.

Mwl. Joyce Macha ni Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Monduli, alifanya mahojiano na jaridi hili hivi karibuni na kueleza kuwa moja ya majukumu ambayo ofisi yake inayapatia msukumo mkubwa kwa sasa ni utoaji wa elimu kwa walimu kuhusu Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji kazi katika Utumishi wa walimu, matumizi ya Mfumo ya kielektroniki ujulikanao kama Teachers' Service Commission Management Information System (TSCMIS), kushughulikia masuala ya ajira, maadili na maendeleo ya walimu.

Akizungumzia kuhusu utoaji elimu juu ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji kazi katika Utumishi wa Walimu, Mwl. Macha alisema zaidi ya walimu 330 wamefikiwa.

Aliongeza kuwa Ofisi hiyo imegawa nakala 88 za kitabu cha Ufafanuzi huo ambapo nakala wamekabidhiwa wakuu wa shule zote za Msingi za Serikali, maafisa elimu kata na ofisi ya Uthibiti Ubora.

"Vilevile, walimu wote Msingi na Sekondari waligawiwa kitabu hicho kwa njia ya nakala laini kwenye vishkwambi vyao. Mikakati yetu ni kuwafikia walimu wote 1,070 kuwapatia elimu kwa kufanya ziara shuleni kabla ya kumalizika kwa mwaka huu wa fedha, yaani mwezi Juni, 2024," alisema Mwl. Macha.

Sambamba na utoaji elimu kwa walimu, TSC Monduli imekuwa mstari wa mbele katika matumizi ya Mfumo mpya wa TSCMIS katika kutoa huduma ambapo usajili wa walimu 13 wa ajira mpya umefanyika kupitia mfumo huo.

Kuhusu kupandisha vyeo, Mwl. Macha alieleza kuwa, katika mwaka wa fedha 2022/2023 TSC Wilaya Monduli iliwapandisha vyeo jumla ya walimu 389 wakiwemo 301 wa shule za Msingi na 88 wa shule za Sekondari ambapo wote wamebadilishiwa mishahara na wamekabidhiwa barua zao.

Kaimu Katibu Msaidizi huyo alisema hali ya nidhamu ya walimu kwa Wilaya hiyo ni ya kuridhisha kwani kwa mwaka 2022/2023 imepokea mashauri



*Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Monduli, Mwl. Joyce Macha akiongea katika kikao cha watumishi wa ofisi hiyo na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali wa TSC Makao Makuu, Gerard Chami wakati wa ziara ya Mkuu huyo wa Kitengo aliyoifanya Wilayani Monduli hivi karibuni.*

ya nidhamu 10 huku mwaka 2021/2022 mashauri Matano (5) yalifunguliwa na mwaka 2020/2021 mashauri Matano (5) ndiyo yaliyofunguliwa.

"Kati ya mashauri 10 yaliyo wasilishwa mwaka 2022/2023 mashauri 6 yamehitimishwa na mashauri 4 yanasubiri uteuzi wa Kamati za Wilaya ili yaweze kuhitimishwa," alisema Macha.

Akitoa sababu za kuongezeka kwa mashauri ya nidhamu kwa mwaka 2022/2023, Macha alisema kuwa ilitokana na mwajiri kuleta tuhuma za walimu 4 watoro (walioacha kazi bila utaratibu) wa muda mrefu kwa ajili ya kuhitimisha mashauri yao ili waondolewe kwenye mfumo wa malipo ya mshahara.

Pamoja na mafanikio mbalimbali yaliyopatikana, Kaimu katibu Msaidizi huyo alitoa mapendekezo ya kumaliza changamoto za utendaji kazi katika ofisi hiyo ikiwemo watumishi wa ofisi hiyo kupatiwa mafunzo ya matumizi ya mfumo wa TSCMIS ili kuweza kutuo huduma zote zikiwemo upandishaji vyeo, ushughulikiaji wa mashauri ya nidhamu na ubadilishaji wa kazi kwa kutumia mfumo huo.

Pia, ameomba mazingira ya ofisi hiyo yaweze kuboreshwa kwa kupatiwa vitendea kazi ikiwemo kompyuta na printa, ukarabati wa vyumba vya ofisi, kupatiwa usafiri wa uhakika kwa ajili ya kufanya ziara shuleni pamoja na kuwezeshwa kupata kibao cha kuitambulisha ofisi hiyo. Ofisi ina upungufu wa vitendea kazi ambavyo ni Kompyuta mbili na Printa mbili.



*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali wa TSC Makao Makuu, Gerard Chami akizungumza wakati wa kikao chake na watumishi wa TSC Wilaya ya Monduli kilichofanyika hivi karibuni.*



*Mmoja wa watumishi wa TSC Wilaya ya Monduli akichangia jambo wakati wa kikao cha watumishi wa ofisi hiyo na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali wa TSC Makao Makuu, Gerard Chami wakati wa ziara ya Mkuu huyo wa Kitengo aliyoifanya Wilayani Monduli hivi karibuni.*




*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali wa TSC Makao Makuu, Gerard Chami (wa pili kutoka kulia) akiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa TSC Wilaya ya Monduli wakati wa ziara yake aliyoifanya wilayani hapo hivi karibuni.*



*Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Arumeru, Bi Zeituni Kinkwerema akiongea katika kikao cha watumishi wa ofisi hiyo na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali wa TSC Makao Makuu, Gerard Chami (hawapo pichani) wakati wa ziara ya Mkuu huyo wa Kitengo aliyoifanya Wilayani Arumeru hivi karibuni.*



*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali wa TSC Makao Makuu, Gerard Chami (wa pili kutoka kushoto) akizungumza wakatia wa kikao chake na watumishi wa TSC Wilaya ya Arumeru kilichofanyika hivi karibuni.*



*Watumishi wa TSC Wilaya ya Arumeru wakiwa katika kikao na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali wa TSC Makao Makuu, Gerard Chami (hayupo pichani) kilichofanyika hivi karibuni katika Ofisi za TSC Wilaya ya Arumeru.*



*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali wa TSC Makao Makuu, Gerard Chami (wa pili kutoka kushoto) akiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa TSC Wilaya ya Arumeru wakati wa ziara yake aliyoifanya katika ofisi hiyo hivi karibuni. Pichani, katikati ni Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Arumeru, Bi Zeituni Kinkwerema.*

# VIONGOZI WA MICHEZO TSC WATAKIWA KUTAFUTA WAFADHILI KUWEZESHA USHIRIKI WA WANAMICHEZO KWENYE MASHINDANO MBALIMBALI

**Na Mwandishi wetu – Dodoma.**



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akiongea na wanamichezo wa TSC (hawapo pichani) wanaoshiriki mashindano ya SHIMIWI kwa mwaka 2023. Kikao hicho kilifanyika tarehe 28 Septemba, 2023 katika Ukumbi wa Mikutano wa TSC jijini Dodoma.*

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama amewataka viongozi wa michezo wa Tume hiyo kufanya jitihada za kutafuta wadau mbalimbali wa kusaidia timu za michezo za TSC kwa kuwa bajeti ya Tume hiyo hawezi kutosheleza mahitaji yote.

Mwl. Nkwama ameyasema hayo Septemba 28, 2023 wakati akiwaaga wachezaji wa timu ya kuvuta kamba (wanaume) na michezo ya ndani ambayo inashiriki mashindano ya SHIMIWI yanayofanyikia mjini Iringa.

Nkwama alisema bajeti ya Tume haiwezi kutosheleza mahitaji ya timu zote kuweza kushiriki mashindano mbalimbali, hivyo imelazimu timu zingine kutoshiriki mashindano hayo muhimu.

"Tulitamani timu zetu zote zishiriki mashindano haya ya SHIMIWI na mashindano mengine yote tunayopaswa kushiriki, lakini kama mnavyojua hali ya kifedha hairuhusu. Hivyo, ni lazima viongozi wa michezo mfanye juhudi kutafuta wadau mbalimbali wanaoweza kusaidia timu zetu. Ninajua hili linawezekana na ninataka mfanye hivyo ili mashindano yanayokuja timu zetu zote ziweze kushiriki," alisema Mwl. Nkwama.

Pamoja na hayo, Katibu huyo amewataka wachezaji hao kujitahidi kufanya vizuri katika mashindano hayo na kuzingatia nidhamu na maadili ya Utumishi wa Umma wakati wote wa mashindano hayo ili kuendelea kuitangaza vyema Tume ya Utumishi wa Walimu.

"Huko kwenye michezo ninataka mkawe mabalozi wazuri wa kuitangaza TSC. Tunahitaji mshinde mrudi na makombe mengi lakini pia kila mmoja akumbuke kuwa yeye ni Mtumishi wa Umma, sote tunafahaamu Miiko na Maadili yetu. Hivyo, ninatarajia kila mmoja atakuwa na nidhamu nzuri na atafanya yale tu yanayokubalika katika utumishi wa Umma," alisisitiza Mwl. Nkwama.

Kwa upande wake Makamu Mwenyekiti wa Michezo TSC, Mwl. Metildis Kapinga alimshukuru Katibu Katibu wa Tume hiyo kwa namna anavyothamini michezo na kuamua kutenga bajeti ya kuwezesha wanamichezo kushiriki mashindano ya SHIMIWI.

"Kwa niaba ya wachezaji wenzangu tunakushukuru sana mwajiri wetu kwa namna unavyotujali sisi wanamichezo. Tunashukuru kwa kutuwezesha kushiriki mashindano haya pamoja na kutupatia vifaa mbalimbali ikiwemo jezi, viatu pamoja na sare za kuvaa siku ya ufunguzi wa mashindano," alisema Mwl. Kapinga.

Aidha, Mwl. Kapinga aliahidi kuwa uongozi wa michezo TSC utatekeleza agizo la Katibu wa Tume la kutafuta wadau mbalimbali wa michezo ili kuweza kusaidia timu nyingi zaidi kushiriki mashindano mbalimbali.



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akiongea na wanamichezo wa TSC wanaoshiriki mashindano ya SHIMIWI kwa mwaka 2023. Kikao hicho kilifanyika tarehe 28 Septemba, 2023 katika Ukumbi wa Mikutano wa TSC jijini Dodoma.*



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akiongea na wanamichezo wa TSC wanaoshiriki mashindano ya SHIMIWI kwa mwaka 2023. Kikao hicho kilifanyika tarehe 28 Septemba, 2023 katika Ukumbi wa Mikutano wa TSC jijini Dodoma.*



*Wanamichezo wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wakimsikiza Katibu wa Tume hiyo, Mwl. Paulina Nkwama wakati wa kikao cha kuagana kabla ya kusafiri kwenda Iringa kwenye mashindano ya SHIMIWI. Kikao hicho kilifanyika tarehe 28 Septemba, 2023 katika Ukumbi wa Mikutano wa TSC jijini Dodoma.*









*Wachezaji wa timu ya Kamba ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) katika mashindano ya SHIMIWI kwa mwaka 2023 wakiwa katika picha ya pamoja wakati wa mashindano hayo yanayofanyika mjini Iringa.*











*Wachezaji wa timu ya kuvuta kamba ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) katika mashindano ya SHIMIWI kwa mwaka 2023 wakivuta kamba katika mashindano hayo yanayoendelea mjini Iringa.*



**MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA**
**Simu: +255 (26) 2322402-4** **Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz** **Tovuti: www.tsc.go.tz**

Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania tumeyautumishiwawalimutanzania